

# UKWELI WA MADAI



## Ndoa za utotoni

Duniani kote inakadiriwa kwa wasichana milioni 51 wenyе chini ya umri wa miaka 18 wameolewa. Ndoa za umri mdogo zimekithiri Afrika Mashariki na Asia ya Kusini. Muongo ujao zaidi ya wasichana milioni 100 watakuwa wamekumbwa na ndoa za umri mdogo.

- Tanzania ni moja ya nchi zilizokithiri kwa ndoa za umri mdogo duniani. Kwa wastani, wasichana wawili kati ya watano huolewa kabla hawajatimiza miaka 18. Mwaka 2010, asilimia 37 ya wanawake wenyе umri wa miaka 20 hadi 24 walioolewa kabla ya kufikia miaka 18. Takwimu zinzonyesha kwamba kupungua kwa asilimia 10 tangu mwaka 2004 (asilimia 41).
- Wakati ndoa za umri mdogo zinaonekana ni kitu cha kawaida nchini Tanzania, Mikoa inayoongoza kwa ndoa hizo ni Shinyanga (asilimia 59), Tabora (asilimia 58), Mara (asilimia 55), Dodoma (asilimia 51), Lindi (asilimia 48), Mbeya (asilimia 45), Morogoro (asilimia 42), Rukwa (asilimia 40), Ruvuma (asilimia 39), Mwanza (asilimia 37), Kagera (asilimia 36), Mtwara (asilimia 35), Manyara (asilimia 34), Pwani (asilimia 33), Tanga (asilimia 29), Arusha (asilimia 27), Kilimanjaro (asilimia 27), Kigoma (asilimia 26), Dar es Salaam asilimia 19), na Iringa (asilimia 8).
- Familia za wahalifu wa ukatili wa kijinsia pamoja na waathirika huamua kumaliza mogororo kwa kuoana, ikiwa na maana kwamba mwathirika huolewa na mbakaji. Ni lazima ielewewe kwamba ndoa za lazima ni haramu nchimi Tanzania.
- Kati ya wasichana 10 kisiwani Pemba, watano huacha shule.
- Sheria ya ndoa ya mwaka 1971 haiwalindi wasichana dhidi ya kuolewa. Sheria hii imekuwa ikipigwa kelele ifanyiwe marekebisho kwa mda mrefu. Sheria hii inaruhusu wasichana wenyе miaka 14 kuolewa kwa (ruhusa maalum ya wazazi), inaruhusu wasichana wenyе umri kuanzia miaka 15 kuolewa iwapo umbile lao linaonekana kubwa. Hali hii ina athari kwa maendeleo ya Taifa.
- Ndoa za umri mdogo ni aina ya ubaguzi wa kijinsia ambao unawagusa wasichana wadogo na kuwafanya wasiendelee na elimu. Ubaguzi huo unawafanya wawe waathirika wa kuambukizwa virusi vya ukimwi kwa urahisi wakilinganishwa na wenzao ambaо hawajaolewa; na hakuna uwezekano wa wasichana hao walioolewa kupanga uzazi.
- Ndoa za umri mdogo ni suala la afya pamoja na ukiukwaji wa haki za binadamu, kwani wasichana walioolewa kwa umri mdogo wana uwezekano mkubwa wa kuathiriwa na fistula na vifo vya kina mama kwani miili yao inakuwa bado haijawa na uwezo wa kuhimili mzigo wa kuzaa.

### ATHARI ZA NDOA ZA UMRI MDOGO

- Zinaongeza kiwango cha vifo vya mama na mtoto
- Tofauti ya umri kwa ndoa za utotoni inaongeza athari ya maambukizo ya UKIMWI
- Hakuna msaada kwa wasichana walioathiriwa na ndoa za umri mdogo kwa sababu wengi wao hutengwa
- Ukosefu wa elimu.

Mara nyingi ndoa za umri mdogo huwakumba wasichana wenyе elimu ndogo au wasio na elimu kabisa. Ndoa za aina hii zimekithiri zaidi vijijini

ambako wananchi wengi wana maisha duni. Mwaka 2010, wanawake wenyе umri wa miaka 20 – 24 wanaishi vijijini walikuwa na uwezekano mkubwa na kuolewa kabla ya kutimiza miaka 18 ikilinganishwa na wenzao waishio mijini. Uwiano huu wa vijijini na mijini umebacki katika kiwango kile kile tangu mwaka 2004. Ukosefu wa elimu unahuishwa zaidi na uwapo wa ndoa za utotoni nchini Tanzania. Asilimia 61 ya wanawake wenyе umri wa miaka 20 – 24 hawana elimu na asilimia 39 wana elimu ya msingi na walioolewa wakiwa na umri wa miaka 18, ikilinganishwa na asilimia 5 ya wale wenyе elimu ya sekondari au vyuo vya elimu ya juu.

### NDOA ZA UMRI MDOGO HUFANYIKA WAPI?

- Aina ya ndoa hizi zimeenea zaidi vijijini mionganii mwa familia maskini. Wakati mwingine wazazi huamini kwamba ndoa hizo zinawalinda wasichana, wengine huamini kuwa zinasaidia kulinda familia ya mhusika kwa kuipatia kipato kitokanacho na mahari; hata hivyo, wakati mwingine wasichana hawa hutumiwa kama bidhaa.
- Nchini Ethiopia na baadhi ya sehemu za Afrika Magharibi, wasichana huolewa wakiwa na umri wa miaka saba.
- Nchini Bangladesh, asilimia 45 ya wanawake wenyе umri kati ya miaka 25 na 29 wameolewa.
- Wasichana wenyе elimu kubwa wana uwezekano mdogo wa kunaswa katika lindi la ndoa za umri mdogo. Nchini Msambiji, asilimia 60 ya wasichana ambaо hawana elimu huolewa wakishafikia miaka 18 ikilinganishwa na asilimia 10 ya wale wenyе elimu ya sekondari na asilimia moja ya wale wenyе elimu ya juu.
- Elimu kwa wasichana ni kigezo muhimu cha kuongeza umri wa kuolewa katika nchi zinazoendelea kama vile Indonesia, Sri Lanka, Taiwan na Thailand.

### KWA NINI MILA HII HUTEKELEZWA?

- Ni kwa sababu ya umaskini na ubaguzi wa kijinsia
- Ni kwa sababu za kijamii, kitamaduni na kiuchumi
- Kiwango kikubwa cha umaskini, vifo na uzazi
- Kiwango duni cha maendeleo, ikiwemo elimu, ajira na afya.

### NINI KIMEFANYIKA KUPAMBANA NA NDOA ZA UMRI MDOGO

- Kampeni ya kurekebishesha kwa sheria ya Ndoa 1971 kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Haki za Binadamu, Hellen Kijo Bisimba, "hii ni kazi nzito ambayo nimeipigania bila mafanikio tangu nimekuwa nikifanya kazi ya uanaharakati."
- Elimu endelevu kwa kutumia vyombo vya habari, utafiti, mabadiliko ya sheria na mikutano ya kijamii.
- Elimu kwa viongozi wa kijamii kuhusu athari za ndoa za utotoni na sheria zilizopo
- Sekta ya afya ihamasishe wananchi kuhusu athari za ndoa za umri mdogo.
- Kuwalusisha viongozi wa dini katika kuielimisha jamii
- Kuzihusisha shule kuhusu madhara ya ndoa za umri mdogo
- Hivi sasa wasichana wana elimu pana kuhusu haki zao
- Wazazi washirikiane na serikali kukomesha ndoa hizo.

# Ukeketaji



- UKEKETAJI** huelezwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kama "taratibu zozote zinazohusu ama kukatwa kidogo au kabisa kwa viungo vya nje vya uke au kuharibiwa kwa viungo hivyo kwa sababu zisizo za kitabibu."
- Sheria ya Makosa ya Kujamiana ya mwaka 1998 Sura ya Pili Kifungu 21 ilirekebisha kifungu 169 A ya Kesi ya Jinai imepiga marufuku mila ya ukeketaji ili kuzuia ukatili dhidi ya watoto. Sheria hii inamaanisha kuwa mtu yoyote atakayepatikana amemkeketa kisiri msichana mwenye umri wa miaka chini ya 18 atahesabiwa kuwa ametenda kosa la ukatili kwa watoto. (kwa maneno mengine kosa hili halihusu wanawake wenye umri zaidi ya miaka 18).
- Katika Wilaya ya Singida Vijijini, asilimia 95 ya wanawake wanaojifungulia hospitalini wamekeketwa (TAMWA 2012). Wanaamini kwamba ukeketaji ni tiba ya ugonjwa unaoitwa 'lawalawa' ambao huwaathiri wasichana wadogo. Utafiti wa TAMWA pia unaonyesha kwamba magadi hutumika katika ukeketaji wa watoto wachanga mkoani Singida.
- Mkoani Mara, taarifa za mashirika ya kiraia zinaonyesha kwamba wasichana wanane wenye afya safi walikufa baada ya kukeketwa

na kupoteza damu nyingi miezi miwili iliyopita. Taarifa nyingine zinadai kwamba wasichana hutolewa kafara wakati wa kuanza kwa msimimu wa ukeketaji kuridhisha miungu ya kijadi.

## INAFANYIKA WAPI DUNIANI?

- Mila hii imeenea Afrika ya Kat, Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, na baadhi ya nchi za Mashariki ya kat. Wanawake wengi waliokeketwa wanaishi katika nchi 28 za Afrika na Mashariki ya kat. Karibu nusu ya wanawake waliokeketwa wanaishi Misri na Ethiopia. (Nchini Misri, utafiti wa afya wa 2008 unaonyesha kwamba mila hiyo sasa imeanza kutoweka).

- Kwa kiwango kidogo, mila hiyo hufanyika Indonesia, Malaysia, Pakistani na India. Baadhi ya wahamiaji wanaendeleza mila hiyo sehemu mbalimbali duniani, zikiwemo nchi za Australia, Canada, New Zealand, Marekani na baadhi ya mataifa ya Ulaya .

## KWA NINI INAFANYIKA?

Zipo sababu nyingi kwanini mila hii huendelezwa .sababu hizo ni pamoa na zile za kijamii, kiuchumi, kisiasa na kidini, ingawa hakuna msaafu wowote unaosema hivyo. Zipo imani kadhaa kuhusu jambo hilo kama vile:

- Kwamba kinembe kitaendelea kukua jinsi msichana anavyokua, na kwa hiyo ni lazima kiondolewe.
- Kudhibiti hamu ya wanawake kufanya mapezni na kutunza ubikira hadi wakati wa ndoa na pia kuwepo uaminifu katika ndoa.
- Kumfanya msichana akubalike katika jamii na kuongeza uwezekano wa kuolewa kwake
- Ni sehemu ya kuonyesha kwamba msichana sasa ni mtu mzima.
- Ukeketaji unahusishwa na imani kwamba msichana sasa ni mwanamke wa kuvutia, mrembo na msafi
- Kinembe kisipokatwa kitakua na kufanana na dhakari
- Mtoto atakufa iwapo atagusa kinembe wakati wa kuzaliwa

## NINI KIMEFANYIKA KUHUSU UKEKETAJI?

- Kuelimisha jamii kuitia mikutano na mafunzo kuhusu haki za binadamu;
- Kuhusisha wadau kuhusu kubadili tabia;
- Kuangalia mila mbadala ya kukua kwa msichana kama iliyvo katika kijiji cha Masanga wilayani Tarime, na kazi iliyofanya na NAFGEM.

## Kuenea kwa mila ya UKEKETAJI KWA ULINGANISHO WA MIKOZA TANZANIA.

Na.	Mkoa	Asilimia
1	Manyara	70.8
2	Dodoma	63.8
3	Arusha	58.6
4	Singida	51.0
5	Mara	39.0
6	Morogoro	21.0
7	Kilimanjaro	21.0
8	Tanga	19.0

Chanzo: Network Against Female Genital Multilation (NAFGEM)